TAREKHE YA WANAVYUONI WA ZANZIBAR

SHEIKH ABUBAKAR BIN ABDALLAH BAKATHIR

(1298– 1362 AH/1881 – 1943 AD)

SHEIKH ABUBAKAR BIN ABDALLAH BAKATHIR

Jina lake

Sheikh Abubakar bin Abdallah bin Muhammad bin Salim bin Ahmad bin Ali bin Abdallah bin Omar bin Kadhi Abdur-Rahim Bakathir Al-Kindy.

Wazee wake

Babu yakewa pili Bwana Salim bin Ahmad ndie aliyehamia Afrika ya Mashariki na akaja akazaliwa babu yake bwana Muhammad huko kisiwa cha Lamu. Ama babu yake Kadhi Abdur-Rahim alikuwa ni Kadhi wa Tarim mji maarufu Hadhramout kwa Wanavyuoni tokea kale. Watu wa ukoo huu wa Al-Kindy wapo zaidi maeneo ya Hadhramout na Oman.

Kuzaliwa na kulelewa kwake

Sheikh Abubakar Bakathir amezaliwa mwezi wa Shaabani mwaka 1298AH sawa na 1881AD.

Alilelewa na baba yake mzazi Sheikh Abdallah Bakathir na akapata malezi yaliyo bora kabisa.

Kusoma kwake

Sheikh Abubakar alisoma kwa Mashekhe wengi sana, amepokea Ijaza nyingi kutoka kwa Wanavyuoni wa Hadhramout alipokuwa na baba yake katika ile safari yake maarufu ambayo imenukuliwa na kuwekwa katika maandishi.

Sheikh Abubakar amesoma zaidi kwa baba yake Sheikh Abdallah Bakathir. Sheikh Abdallah Bakathir alikuwa na madarsa mengi sana wakati wake na wanafunzi wa rika tofauti walikuwa wakihudhuria darasa zake. Sheikh Abubakar pia amesoma fani ya Mustalahi kwa Sheikh Al-Amin wa Mombasa.

Mashekhe zake wa Lamu

Lamu katika zama hizo walijaa Wanavyuoni na Wacha-Mungu, hivyo alibahatika kusoma tokea utotoni mwake kwa Mabwana hao walio mashuhuri sana ambao ndio mashekhe wakubwa wa baba yake, ijapokuwa hakupata

kusoma sana kwao kwani alihamia unguja pale baba yake alipofanya mskani yake Unguja.

Miongoni mwa Mashekhe wake wa Lamu:

1. Sayyid Abubakar Abdur-Rahman Al-Husayny maarufu (Mansab).
2. Sayyid Ali bin Abdallah bin Hasan Jamalil Leyl.
3. Habib Saleh bin Alwy bin Abdallah Jamalil Leyl, (alisoma Tafsiri ya Quran).
4. Sheikh Muhammad bin Ali bin Mselem Al-Amiry (Kadhi wa Lamu).
5. Sheikh Abubakar bin Muhammad Al-Maawy.

Mashekhe wake wa Makka

Sheikh Abubakar alikwenda Makka mwaka 1314 AH (1923) na akakaa huko kwa muda wa miezi 6 akisoma kwa Wanavyuoni waliokuwepo zama hizona alipata bahati ya kusoma kwa baadhi ya wale Mashekhe waliomsomesha baba yake.

Miongoni mwa Mashekhe wa baba yake wa Makka ni:

1. Sheikh Omar bin Abubakar Bajuneyd.
2. Sheikh Muhammad Said bin Muhammad Babsyl (Mufti wa Makka).
3. Habib Husein bin Muhammad bin Husein Al-Hibshy (alikuwa Mufti wa Makka wa zama zake).

Mashekhe zake wa Hadhramout

Sheikh Abubakar amebahatika kufatana na baba yake Sheikh Abdallah katika safari ya kuelekea Hadhramout ambayo Sheikh Abdallah alifuatana na sahibu yake Sayyid Abubakar bin Ahmad bin Sheikh Patte, mwanawe Sheikh Abubakar bin Abdallah Bakathir na Sheikh Muawiya bin Hasan Al-Maawy mtoto wa mama yake mdogo.

Safari hii ilikuwa mwezi 21 Mfungo mosi 1314 AH sawa na tarehe 26 March 1897. Sheikh Abdallah alipita kila maeneo ya Mabwana watukufu na kutabaruku kwa kusoma baadhi ya vitabu mbele yao na kupatiwa Ijaza tele ambapo na yeye Sheikh Abubakar akihudhuria, hivyo kila Ijaza alizopewa baba yake kutoka kwa mabwana wakubwa basi na yeye kapewa.

Miongoni mwa Mashekhe aliosoma Sheikh Abadallah vitabu mbele yao:

1. Habib Ali bin Muhammad Al-Hibshy (wa Seyun).
2. Habib Tahir bin Abdallah bin Sumeit (wa Shibam).
3. Habib Abdur-Rahman bin Muhammad Al-Mashuhur (wa Tareem na aliyekuwa Mufti wa Hadhramout).
4. Sheikh Muhammad Baridhwan (wa Inaat).
5. Sayyid Ahmad bin Muhammad Al-Kaaf (wa Tareem).
6. Sheikh Ahmad bin Abdallah Al-Khatiib (wa Tareem).
7. Habib Ubaydillah bin Muhsin Assaqqaf (wa Seyun) na
8. Habib Ahmad bin Hasan Al-Attas (wa Hureidha).

Ama Ijaza alizopewa Sheikh Abdallah pamoja na aliofatana nao kutoka kwa Mashekhe tofauti amezitaja katika kitabu cha safari yake hiyo kinachoitwa *Al-Ashwaqul Qawiyyah ilaa Mawatini Saadatil Alawiyah,* kitabu hiki kimechapishwa na kinapatikana katika mtandao pia.

Kusomesha kwake

Sheikh Abubakar alisomesha sana Unguja na alikuwa na wanafunzi wengi, alisomesha vitabu tofauti na fani mbalimbali. Alikuwa na darsa za kila wakati, alisomesha nyumbani kwake, Msikiti Gofu, Madrasaaliyoanzisha baba yake ya Ukutani pamoja na Msikiti Baraza.

Alikuwa mahiri wa kutowa mawaidha, watu wakipenda kusikiliza mawaidha yake. Darasa za Msikiti Gofu khasa zile za Ramadhani zilinawiri wakati wake, adhuhuri akisomesha kitabu maarufu cha cha Tasawwuf *Ihyaa ulumid-ddin* cha Abu Hamid Muhammad ibn al-Ghazali (Imam Ghazali) na vitabu vyengine na jioni akisomesha Tafsiri ya *Jalaleyn.*

Sheikh Abubakar pamoja na Sheikh Muhsin bin Barwani ndio waliotawalishwa na Habib Ahmad bin Sumeyt na kupewa makamo ya kusomesha Msikiti Gofu katika mwezi wa Ramadhani baada ya kufariki Sheikh Abdallah Bakathir na hivi ndivyo ilivyokuwa namna ya kutangulizwa mtu na Mashekhe kudarasisha katika Msikiti Gofu. Pia kulikuwa na nidhamu ya kutalii kwa pamoja baadhi ya Mashekhe pamoja na mdarisishaji kabla ya darasa

kama walivyokuwa wakitalii pamoja Sheikh Muhsin bin Ali Barwany, Sheikh Abubakar Bakathir na Sheikh Muhammad bin Omar.

Pia katika darasa zake za siku za kula mchana akisomesha Tafsiri ya *Quran*, fani za Lugha khasa Nahawu, Fik-hi, fani za Hadithi na Tasawwuf. Alikuwa akidarasisha tokea baba yake yupo hai kwa amri ya baba yake na alimwambia asomeshe Nahwu kabla ya darsa kubwa ya Fik-hi.

Katika baadhi ya darasa zake walikuwa wakihudhuria baadhi ya wanafunzi waliokuwa wa baba yake na kustafidi kutoka kwake pia.

Miongoni mwa wanafunzi wake wakubwa ni:

1. Sheikh Yusuf bin Ali Shirazy.
2. Sheikh Suleyman bin Muhammad Alawy.
3. Sheikh Abdallah Saleh Farsy.
4. Pamoja na baadhi ya wanafunzi wa baba yake.

Madhehebu yake

Sheikh Abubakar alikuwa na itikadi ya Ahlu Sunna Wal-Jamaah, akifuata madhehebu ya Kishafii katika Fik-hi, na akifuata Tariqa ya Aal-Baalawy katika Tasawwuf.

Vitabu alivyotunga

Sheikh Abubakar hakuwa na vitabu vingi alivyoviandika, muda wake mwingi alikuwa akiutumia katika kudarasisha. Alipata kutunga kitabu kimoja cha Kiswahili kuwarejeza Makadiani alichokiita *Nasaihud-diniyya*.

Safari zake

Sheikh Abubakar alipata kusafiri kwenda Hadhramout na baba yake na pia alikwenda Makka na akakaa huko kwa muda wa miezi sita akisoma kwa Wanavyuoni mbalimbali wa Makka.

Mafungamano yake na Wanavyuoni

Sheikh Abubakar alikuwa kipenzi cha Mashekhe waliomsomesha, alipendwa na kuthaminiwa nae aliwapenda wanafunzi wenzake ambao baadae ndio waliokuwa Wanavyuoni katika wakati wao.

Alipendwa sana na mashekhe wa Hadhramout katiak ile safari yake na baba yake, wengine walipozuru Unguja hawakuwacha kumtembelea na kuwa nae katika madarsa yake mfano wa hao ni Habib Salim bin Hafiidh.

Habib Salim bin Hafiidh alizuru Unguja mwaka 1358 na kupokewa na Habib Omar bin Sumeyt, alihudhuria majlisi za kheri nyingi na kuthibitishwa kimaandishi pamoja na Ijaza alizotowa au kupeana na Wanavyuoni. Ameyaandika hayo Habib Omar bin Sumeyt na kuiita ziara hiyo *Shadhiyil-Azhaar.*

Habib Salim bin Hafiidh alihudhuria baadhi ya darsa za Sheikh Abubakar Bakathir, pia alitowa Ijaza kwa waliohudhuria darsa za Sheikh Abubakar Bakathir.

Miongoni mwa darsa za Sheikh Abubakar alizohudhuria Habib Salim bin Hafiidh:

1. Alihudhuria nyumbani kwa Sheikh Abubakar siku ya kukhitimisha kitabu cha Imamul Haddad *Addaawatu-Tammah* na kitabu *Al-Manhajul-Qawiim k*itabu cha fik-hi sherehe ya *Muqaddimatul Hadhramiyya* (Robo) iliyotungwa na Imam Ibn Hajar Haytamy.
2. Alihudhuria darsa ya kukhitimisha kitabu *Risalatul-Mudhakarah* cha Imamul Haddad.
3. Alihudhuria darsa ya siku ya kuanza kitabu *Risalatul-Muawanah* cha Imamul Haddad.
4. Alihudhuria Rawha ya laasiri siku ya Ijumaa mwezi 29 Rabiul Awwal ilikuwa Msikiti Baraza na palikuwa panasomwa vitabu vya Imamul Haddad na kitabu *Al-Uhudul-Muhammadiyyah* cha Imam Shaarany.

Vitabu vya Imamul Haddad

Utaona angalabu ya vitabu vilivyotajwa ni vya Tawassuf tena vya Imamul Haddad, hii inaashiria kuwa Sheikh Abubakar na Mashekhe wa Unguja walishikamana na Tariqa ya Aal-Baalawy zaidi.

Vitabu vya Imamul Haddad vina barka na faida kubwa kwa anaevisoma. Imamul Haddad amekusanya faida kutoka chungu ya vitabu kwa lugha nyepesi kabisa anaifahamu kila anaefahamu lugha ya kiarabu.

Pamoja na vitabu hivyo vilivyotajwa hapo juu kuna kitabu kikubwa cha Imamul Haddad ambacho huwa kinasomeshwa mara kwa mara kinachoitwa *Annasaihud-Diiniyyah,* hiki ni kitabu chake kikubwa, amekitunga kufupisha yaliyomo katika kitabu kikubwa cha Tasawwuf cha Imamul Ghazali *Ihyaa Ulumid-diin.*

Wanavyuoni wote wa Aal-Baalawy wamekubaliana kuwa Imamul Haddad ni Mujjaddid wa Tariqa hiyo na vitabu vyake hivyo na vyengine ndio nguzo na mwenendo unaopaswa kufuatwa na kila mmoja kati yao.

Aghalabu ya vitabu hivyo husomwa kwa njia ya Sard yaani husoma mwanafunzi mmoja wengine husikiliza na Sheikh hutia sherehe sehemu aitakayo.

Mtindo huu wa usomaji kwa vitabu vya Tasawwuf au vya Manaqib umezoeleka huko Hadhramout na hupatikana fursa ya kusomwa vitabu vingi sana kwa wakati mdogo, lakini inahitaji wanaosoma wawe ni waelewa wa kile wanachokisoma.

Rawha nayo iliyotanjwa hapo juu ndio mtindo wa Rawha unaojulikana Hadhramout nao ni kusomwa vitabu mbalimbali na khasa vya Tasawwuf kwa njia ya Sard. Pia wapo baadhi wanaoita uradi wa laasiri kuwa ni Rawha lakini hilo sio Mash-huri kwa Hadhramout.

Sifa zake

Sheikh Abubakar alisifika kwa ukarimu, upole, akipenda wanafunzi wake, alikuwa na Tawadhui, hakuwa akijikweza, alikuwa na himma kubwa ya kusomesha watu na sifa nyenginezo nzuri alizokuwa nazo.

Kufariki kwake

Sheikh Abubakar amefariki alipokuwa sehemu anayodarisisha ghafla wakati wa magharibi usiku wa kuamkia mwezi 14 Shawwal mwaka 1362 AH (13/10/1943) baada ya kuhudhuria Hawli ya Habib Ahmad bin Sumeyt inayofanyika msikiti wa Ijumaa Malindi kila mwezi 13 Shawwal baada ya sala ya Laasiri na kupata fursa ya kulahiqiana na watu wengi wa kheri hapo, kumbe ilikuwa ni sehemu ya kuagana.

Amezikwa pembeni mwa kaburi la baba yake katika kitalu cha Aal- Sheikh kilichopo nyuma ya Ukutani na Wanavyuoni walitunga mashairi ya huzni (Marathi) ya kifo chake.

Watoto wake

Sheikh Abubakar amewacha mtoto mmoja wa kiume Maalim Abdallah Bakathir ambae alisomesha Madrasa watu wengi wa mji wa Unguja katika Madrsatu Nuur iliyopo hapo Ukutani. Pia anakuwa ni mjomba wa Sayyid Ali Badawy, Sharif Dini na Sharifu Khitamu wote wa Lamu.

Rejea

1. Sheikh Abdallah Saleh Farsy *Baadhi ya Wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika* cha mwaka 1972.
2. *Al-Ashwaqul Qawiyyah* ziara ya Sheikh Abdallah Bakathir ya Hadhramout.
3. *Minhatul-ilaah* cha Habib Salim bin Hafiidh kuwataja Mashekhe aliowadiriki.
4. *Shadhiyil-Azhaar z*iara ya Habib Salim bin Hafiidh ya Unguja iliyokusanywa na Habib Omar bin Sumeyt.

Maahad Juneyd Islamiy (2018)

Kitengo cha Bahthi na Utafiti

+255 777 878 047 – Zanzibar